**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA WAZIRI MKUU – TAMISEMI**
**HALMASHAURI YA MJI GEITA**
**MWATULOLE SEC - JOINING INSTRUCTION 2026/2027.**

**MAWASILIANO:**
Mkuu wa shule: 0756434667
Makamu Mkuu wa Shule: 0626057887 / 0752589787
Patron : 0764778204
Email.mwatulolesecondary@gmail.com

**Shule Ya Sekondari Mwatulole,**
S.L. P 635.
**Geita.**

Tarehe: ………………………….

Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi………………………………………..
S.L.P………………………………………………………………

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI MWATULOLE- HALMASHAURI YA MJI- GEITA MWAKA ........ MCHEPUO WA HKL ☐ HGL ☐**

**1.** Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha tano katika shule hii mwaka .......... tahasusi ya_________________. Shule ya sekondari Mwatulole ipo Halmashauri ya Mji Geita. Shule ipo Kilometa 3 kusini Mshariki kutoka Stand, Usafiri wa Bajaji nauli Tsh 1,000/= na bodaboda Tsh. 2,000/= hadi shuleni.

Muhula wa masomo unaanza tarehe **..................** hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe **...................** Mwisho wa kuripoti ni tarehe **.....................**

**2. MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA:**

**2.1. Sare ya Shule ni:-**

a) Mashati mawili (2) meupe ya tetron yenye mikono mirefu.
b) Suruali mbili (2) za rangi nyeusi isiyo na michilizi yoyote na yenye mifuko miwili (2) pembeni na nyuma mmoja (1) isiwe "Modal style".
c) Viatu vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi.
d) T-shet (1) rangi ya Dhahabu yenye kora itakayovaliwa siku ya Jumatano darasani.
e) Soksi jozi mbili (2) rangi nyeusi.
f) Mkanda wa kuvalia suruali ni mweusi wa ngozi.
g) Sare ya michezo ni Traksuit ya rangi ya bluu, raba nyeupe, jezi na soksi ndefu (Rangi ya bluu)
h) Nguo za kushindia ni T-sheti ya blue yenye kora nyeusi na suruali nyeusi nyenye Turn up kwa chini.
i) Tracksuit moja (1) ya rangi ya nyeusi itakayovaliwa baada ya muda wa vipindi.
j) Sweta moja (1) la rangi ya kijivu.
k) Tai ndefu ya rangi nyeusi.

**ANGALIZO:**
Nguo tofauti na hizo zilizotajwa hapo juu hazitakiwi kabisa shuleni.

**NB:** Kwa watakao hitaji badhi ya mahitaji yafuatayo yanayoweza patikana shuleni kwa gharama nafuu.

- i Sweta lenye nembo ya shule.
- ii T-shet rangi ya Bluu yenye nembo ya shule.
- iii T-shet rangi ya Dhahabu yenye nembo ya shule.
- iv Tracksuit ya bluu na nyeusi yenye nembo ya shule.

### 2.2. Michango mbalimbali.

Michango mingine iwekwe katika akaunti ya shule inayoitwa " MWATULOLE SEC SELF RELIANCE ACCOUNT: Na. **31001100447**

| NA. | AINA YA MCHANGO | KIASI |
|---|---|---|
| 1 | Mchango wa Uendeshaji wa shule | 65,000/= |
| 2 | Tahadhari | 5,000/= |
| 3 | Nembo ya shule | 5,000/= |
| 4 | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **JUMLA** | **80,000/=** |

## 3. SHERIA NA KANUNI ZA SHULE

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### 3.1. Sheria na Kanuni za Shule

- i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
- ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
- iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku( Preparation);
- iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
- v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
- vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
- vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;

viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**

- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**

- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa**).

**3.2. Makosa yatakayosababisha mwanafunzi kufukuzwa shule.**

i) Wizi
ii) Kutohudhuria masomo / utoro uliokithiri.
iii) Kugoma na kuhamasisha mgomo, kuhatarisha amani ya shule na jamii kwa ujumla.
iv) Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla.
v) Kuharibu mali ya umma kwa makusudi.
vi) Kukutwa au kutoka nje ya shule bila ruhusa maalumu.
vii) Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule.
viii) Kufuga nywele ndefu / ndevu.
ix) Ulevi na unywaji wa pombe na matumizi ya madawa ya kulevya.
x) Uvutaji wa sigara na bangi.
xi) Uasherati, uhusiano wa jinsi moja, kuoa au kuolewa.
xii) Kumpa ujauzito au kusababisha ujauzito ukiwa bado ni mwanafunzi.
xiii) Kushiriki matendo ya uharifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiv) Kutembelea majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni
xv) Kumiliki, kukutwa na simu ya mkononi katika mazingira ya shule
xvi) Kudharau bendera ya Taifa
xvii) Kujihusisha na michezo ya kamali.
xviii) Kufanya jaribio lolote la kujaribu kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu n.k

## 4. MAHITAJI

- ✓ Godoro imara futi $2\frac{1}{2}$ .
- ✓ Shuka pea mbili (rangi ya light bluu).
- ✓ Chandarua $\frac{4}{6}$
- ✓ Ndoo mbili Lita 10
- ✓ Sahani, bakuli, kikombe , kijiko kwaajili ya chakula.
- ✓ Kanda mbili kwaajili ya kuogea tu.
- ✓ **Vifaa vya Usafi**
    - Ufagio wa plastic wa dukani (soft bloom), fyekeo na squeezer – **HKL tu**
    - Mopper, jembe na ufagio wa chelewa wenye mpini – **HGL tu**
- ✓ Shajala moja (file) kwa ajili ya kutunza kumbukumbu za mwanafunzi.
- ✓ Nakala ya cheti cha kuzaliwa au kitambulisho cha uraia.
- ✓ Nakala ya cheti cha matokeo ya kidato cha nne (Result slip).
- ✓ Hati maalumu ya vipimo kutoka kwa daktari.
- ✓ Madaftari makubwa 7 (Counter book Quire 4) na madogo 7.
- ✓ Rim ya karatasi (A4) Mbili kwa Mwaka.
- ✓ Ni lazima kila mwanafunzi aje na **kadi ya Bima ya Afya** ili imsaidie pindi atakapo ugua kama hana atalipia Tsh. **50,400/=** ili apatiwe Bima yake. Fedha hii italipwa shuleni siku ya kwanza atakapo ripoti shuleni.

*Kiambatanisho (a)*

**HALMASHAURI YA MJI GEITA**

**SHULE YA SEKONDARI MWATULOLE,**
**S.L.P 635,**
**GEITA.**

**KUMB. NA. MSS/ ADM/ F.V/ 2021**

## FOMU YA KUKUBALI

Mzazi / Mlezi wa (Jina la mwanafunzi)

______________________________

Mimi …………………………………………. (mwanafunzi) bila shuruti nakubali kutumia nafasi niliyopewa ya kidato cha …………. katika shule ya sekondari Mwatulole. Pia naahidi kutokushiriki kwa namna yoyote ile katika migomo na maandamano yasiyoruhusiwa.

…………………………………                                   …………………………

Saini ya mwanafunzi                                   tarehe

Mimi ……………………………… mzazi / mlezi wa ………………………………….. (Mwanafunzi) nimeyasoma masharti yote ya mwanangu ya kujiunga na shule ya sekondari Mwatulole na ninakubali na kuahidi kwamba mtoto wangu atafuata masharti yote ya shule ikiwa ni pamoja na kutoshiriki kwa namna yoyote katika migomo. Aidha nitahakikisha kuwa mwanangu anamaliza elimu ya kidato cha sita kwa kuwajibika kulipa michango ya shule pamoja na maelekezo mengine yatakayokuwayakitolewa na shule.

…………………………………                                   …………………………

Saini ya mzazi/mlezi                                   tarehe

*Kiambatanisho (b)*

**HALMASHAURI YA MJI GEITA**
**SHULE YA SEKONDARI MWATULOLE**
**MAELEZO BINAFSI YA MWANAFUNZI.**

***FOMU HII IJAZWE NA MWANAFUNZI***

1. Jina kamili ……………………………………………………………………………..
2. Anuani yako kamili ………………………………………………………………………
3. Tarehe ya kuzaliwa, mwezi na mwaka ……………………………………….…
4. Mahali ulipozaliwa ……………………………………………………………....….
5. Dini / Dhehebu…………………………………………………………………..…...
6. Uraia wako …………………………….……………………………….……………...
7. Shule ya sekondari uliyotoka …………………………………………………
8. Jina kamili la mzazi / mlezi ……………………………………………………....…
9. Anwami ya mzazi / mlezi ……………………………………………..……………
10. Mahali anapoishi ……………………………………………………………………..
    Kijiji ……………………………………… Mtaa …………………………………..
    Kata ………………………… Wilaya ………………….. Mkoa …………………

**AHADI**

Mimi ……………………………………………… Kwa utashi na akili yangu timamu ninaikubali nafasi ya masomo niliyopewa, nitakuwa tayari kujiendeleza kimasomo. Nimezisoma, nimezielewa na nitazifuata sharia za shule pamoja na kanuni na taratibu zitakazotolewa. Natambua kuwa nikifukuzwa shule kwa sababu ya kuvunja sheria za shule makusudi nitavunja moyo wa wazazi na wale wote wanaonisaidia, hivyo jamii itanidharau kabisa. Naahidi kuwa na utii kwa Walimu na Wafanyakazi wote waliopo hapa shuleni ili wanipende na kunisaidia zaidi. Sitakuwa tayari kuanzisha kushauri wala kushiriki katika vurugu za aina yoyote hapa shuleni hususani mgomo kwani ni kwenda kinyume na sharia na taratibu za shule. Nitafanyabidii katika masomo na kazi zote za shule.

**MUNGU NISAIDIE**

…………………………………….....        ……………………………….    ……………

JINA NA SAINI YA MWANAFUNZI        SAINI YA MWANAFUNZI        TAREHE

*Kiambatanisho (c)*

**MWATULOLE SECONDARY SCHOOL**
**SCHOOL MEDICAL EXAMINATION FORM**

**MWATULOLE SECONDARY**
**S.L.P 635,**
**GEITA.**
**DATE: …………**

**To Medical Officer**

**…………………………………………….**

**(Full name)**

**NAME OF STUDENT: …………………………………………………………….**
**Please examine the above named student as per Medical examination form below.**

1. Blood count (Red and White) ………………………………………………………
2. Stool examination …………………………………………………………………...
3. Urine analysis ……………………………………………………………………….. 
4. STDS and other V.D …………………………………………………………………. 
5. T.B and Leprosy test ……………………………………………………………….. 
6. Eye test ………………………………………………………………………………
7. Ear test ……………………………………………………………………………….
8. Chest …………………………………………………………………………………
9. Blood Group (Very Crucial) ………………………………………………………...
10. Neuroses ……………………………………………………………………………
11. Speech ……………………………………………………………………………...
12. Bilharziasis ………………………………………………………………………….
13. Asthma ……………………………………………………………………………...
14. Limbs ………………………………………………………………………………..
15. Other serious Disease ……………………………………………………………….

Remarks and additional information e.g physical defects or impairments, infection, chronic or family disease eg. Sickle cell.

………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………

I have examined the above named student and I certify that she is FIT/ NOT FIT to pursue Secondary Education.

Signature …………………………………………… Date ……………………………

Station ……………………………………………………………………………………

Designation and Official Stamp ……………………………………………………….

*Kiambatanisho (d)*

**MAELEZO BINAFSI YA MZAZI / MLEZI**

***Sehemu hii ijazwe na Mzazi / Mlezi***

1. Jina la Mzazi / Mlezi 1: …………………………………….…….. Na. ya Simu ………………..

   2. …………………………………….…….. Na. ya Simu ……….……...
2. Ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni.

| Mzazi: 1 | Mzazi: 2 | Mzazi: 3 | Mzazi: 4 |
|---|---|---|---|

3. Anuani ya mahali anapoishi sasa………………………………………………….
4. Mahali ulipozaliwa mzazi / mlezi ………………………………………………….
5. Kazi ya mzazi / mlezi ………………………………………………………….…
6. Dini au dhehebu la mzazi / mlezi ……………………………………………...…..
7. Uraia Mzazi / Mlezi ……………………………………………………………….

**AHADI YA MZAZI / MLEZI**

- Mimi……………………………………………………….….. ninakubali nafasi aliyopewa mtoto wangu ……………………………………………………..
- Nitashirikiana na Uongozi wa shule katika suala la kumlea, kumwendeleza au kumtia moyo wa kupenda shule.
- Nitamsaidia mtoto wangu vifaa vya shule ambayo havitolewi shuleni ikiwa ni pamoja na karo na michango mingine inayoidhinishwa na Bodi ya shule.
- Nitahakikisha kwamba mtoto wangu anawahi shuleni na pia hachelewi likizoni.
- Nitafuatilia maendeleo yake kwa karibu zaidi ikibidi hata kuonana na walimu wake.

- Ninatambua pia kumchelewesha kufika shuleni siku a kufungua shule kunaweza kusababisha kupoteza nafasi aliyopewa.
- Nitamruhusu / nitamleta mwanafunzi kuripoti akiwa amekamilisha mahitaji yote na karo ya shule.

8. Jina la Balozi ……………………………….……… Saini / Mhuri ……………………
   Tarehe …………………………………… Namba ya Simu ………………………..

9. Jina la Mwenyekiti wa Mtaa / Kijiji ……………………………………………..
   Saini ya M/Mtaa …………………………….……     Tarehe …………………......
   Namba ya simu ……………………………………     Mhuri ……………………….

Saini ya Mzazi / Mlezi 1: ………………………………… Tarehe ………………….

Saini ya Mzazi / Mlezi 2: ………………………………… Tarehe ………………….

NAKUTAKIA MAANDALIZI MEMA

**……………………………….**

**MKUU WA SHULE**

**NB: Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazihusika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFAHUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

- **Mkuu wa shule: 0756434667**
- **Makamu Mkuu wa Shule: 0626057887 / 0752589787**
- **Mwandamizi Taaluma: 0766400921**
- **Mwandamizi Malezi: 0764778204**